# Kigamboni 2022

Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni April- Juni 2022 Toleo Namba 02

## Kigamboni mmefanya vizuri sana zoezi la Anwani za makazi, malizieni vizuri sehemu iliyobaki, Waziri Nape.



Ni kauli ya waziri wa Habari na Mawasiliano Mhe.Nape Nnauye wakati alipokua akitoa maelekezo matatu ya kufanyiwa kazi baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa zoezi la anuani la makazi Wilaya ya Kigamboni kwenye ukumbi wa mkuu wa Wilaya wakati alipokuwa kwenye ziara yake ya kikazi ya kukagua utekelezaji wa zoezi.

***inaendelea UK.1***

Waziri wa Habrai na Mawasilikano Mhe. Nape Nnauye , Naibu Waziri wa TAMISEMI Mhe. David Silinde, Mbunge Mhe. Faustine Ngungulile ,Mkuu wa Wilaya Mhe. Fatma Almasi Nyangassa, Diwani wa Kata ya Kigamboni Mhe. Dotto Msawa wakikagua baadhi ya vibao vya namba za Nyumba kwenye Kata ya Kigamboni wakati wa ziara ya utekelezaji wa anwani za makazi.

Kigamboni kunufaika na uwekezaji mkubwa, Vijana takribani 5000 watarajiwa kupata ajira



**RC Makalla Aipongeza Kigamboni kwa kupata hati safi ,miaka 5 Mfululizo, aelekeza udhibiti wa mapato na 70% kuelekezwa kwenye Miradi ya maendeleo.**



**Mbio za Mwenge wa Uhuru 2022 zilivyofana Kigamboni, Miradi yenye thamani ya Bilion.1.4 yapita bila kipingamizi.**



# KIGAMBONI 2022

## Kigamboni mmefanya vizuri sana zoezi la Anwani za makazi, malizieni vizuri sehemu ilivyobaki, Waziri Nape.

Waziri Nape alisema kuwa Kigamboni imetekeleza vizuri sana katika zoezi hilo na kuwaomba kuendelea kufanya vizuri zaidi katika zoezi lililobaki la kuweka vibao vya namba kwenye kila nyumba na nguzo za barabara .

Waziri Nape aliongeza kwa kusema kuwa baadhi ya maeneo ambayo yanamigogoro ya umiliki kama maeneo ya jeshi, uwekezaji, hospitali na mengineyo ,anwani za makazi hazitawekwa hadi migogoro hiyo itakapopatiwa ufumbuzi kwani kwa kuweka anwani wakati kunamigogoro ni kuhalalisha umiliki kinyume cha taratibu.




Waziri wa Habrai na Mawasilikano Mhe. Nape Nnauye , Naibu Waziri wa TAMISEMI Mhe. David Silinde, Mbunge Mhe. Faustine Ngungulile ,Mkuu wa Wilaya Mhe. Fatma Almasi Nyangassa, Diwani wa Kata ya Kigamboni Mhe. Dotto Msawa na Mtaalamu mmoja wakiwa kwenye moja ya Anwani.

Aidha alisema kuwa viongozi wahakikishe majina ya mitaa yanaamuliwa na wananchi sambamba na kuhakikisha majina yanayotumika yaweze kutunza historia ya eneo husika na viongozi kutakiwa kuhakikisha wanashawishi wananchikuridhia majina yanayoonekana kutunza historia ya maeneo yao.

Waziri aliwataka viongozi kuanzia ngazi ya Wilaya hadi wajumbe wa nyumba kumi kuhakikisha wanahamasisha wananchi kushirki kwenye zoezi hili la anwani za makakazi kwani kuna nyakati zitafika mwananchi hataweza kupata huduma mbalimbali kama asipokuwa na anwani inayomtambulisha.

Naye Naibu Waziri wa TAMISEMI Mhe. David Silinde alitumia fursa hiyo kuzitaka Halmashauri zote nchini kuhakikisha zinakamilisha zoezi la anwani za makazi kabla ya kufikia mei 30 kwani hakuna sababu itakayopelekea Halmashauri yoyote kushindwa kufikia malengo kwakua miongozo ya utekelezaji yote imekwishatolewa ikiwemo ya kutumia fedha za mapato ya ndani.

'Niweke wazi Halmashauri itakayoshindwa kufikia malengo hatutasita kuichukulia hatua za kinidhamu"Alisema Naibu Waziri.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Amosi Makalla alishukru ujio wa Waziri na Naibu Waziri na kusema kuwa kwa ngazi ya Mkoa zoezi limetekeleza kwa namna yake kwani hakuna Wilaya ambayo ipo chini ya asilimia 100 ya utekelezaji na Mkoa upo tayari kutekeleza maagizo yote yaliyotolewa kwa lengo la kuboresha utendaji kazi.

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Fatma Almasi Nyangassa alishukuru kwa ziara ya kikazi ya viongozi iliyolenga kukagua utekelezaji wa zoezi na kuahidi kuyafanyia kazi malelekezo yote yaliyotolewa ili kufikia lengo la Serikali lililowekwa.

Ikumbukwe Kigamboni ilikadiria kuzifikia anuani za nyumba 49,353 anunani zilizoingizwa kwenye mfumo ni 58,508 sawa na 118.5%, Makadirio ya barabara yalikuwa 1,864 na zilizoingizwa kwenye mfumo 3,617, idadi ya barabara zilizowekwa nguzo ni 85 ambapo 26 zimewekwa katika zoezi hili na 59 ziliwekwa na Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) mwaka 2018. Jumla ya namba za majengo ya makazi na Ofisi za Serikali 47 zimewekwa.Aidha Wilaya ya Kigamboni ilishika nafasi ya kwanza katika zoezi la Ukusanyaji wa taarifa za Anuani na Makazi.

## Vijana Takribani 5000 kunufaika na uwekezaji Kigamboni



**Viongozi wakishuhudia tukio la kusaini mkataba wa mauziano ya eneo la square mita za mraba mil.2.2 lililopo Kisarawe II Kigamboni kwa ajili ya uwekezaji mkubwa wa Kongani ya Viwanda**

Hayo yalibainishwa 9/3/2022 na Waziri wa Uwekezaji,Viwanda na biashara Mhe.Dkt.Ashatu Kijaji katika ukumbi wa Wilaya ya Kigamboni wakati wa tukio la kusaini mkataba wa mauziano ya eneo la square mita za mraba mil.2.2 lililopo Kisarawe II Kigamboni kwa ajili ya uwekezaji mkubwa wa Kongani ya Viwanda ambao haujawahi kutokea kati ya property international na kampuni ya Elsewedy ya Egypt.

Akizungumza katika hafla hiyo ya utiaji saini mkataba wa mauziano ili utekelezaji wa mradi uanze Mhe. Dkt.Ashatu Kijaji alisema mafanikio hayo ya mchakato wa kuanza kutekelezwa kwa mradi huo ni matokeo ya jitihada za Mhe.Rais Samia Suluhu Hassan ambapo amekuwa akiifungua Tanzania kiuchumi toka aingie madarakani.

Aidha alisema mradi huo unaenda kuifanya kigamboni kuwa tajiri kutokana na mapato yatakayopatikana kutoka katika Viwanda vitakavyowekezwa katika eneo hilo ikiwepo Viwanda vya nguo,Viwanda vya kuunganisha magari ,kiwanda cha madawa ambapo tayari mwekezaji wa kiwanda cha hicho ameshasaini mkataba na Elsewedy Kwa ajili ya kuja kuwekeza katika eneo hili ,pamoja na hayo fursa za ajira zitakazopatikana kwa uwekezaji huu ni ajira 50,000.

Mhe Waziri aliwataka watendaji kujiandaa na kazi hiyo njema na wananchi kufanya jitihada kuchukua fursa hii adimu kwani ni ya uhakika kwa kuwa tayari masoko ya uwekezaji huu yapo nje ya nchi Jambo ambalo litaiingizia nchi yetu fedha za kigeni.

Kwa upande wa miundo mbinu rafiki kuelekea eneo la mradi alisema Serikali tayari imetenga fedha kwa ajili ya kujenga barabara ya lami ya kilometa 11 kutoka Kisarawe II na utekelezaji utaanza mara moja ili Kurahisisha utekelezaji wa mradi.

Nae katibu Mkuu wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Prof.Godius Kahyarara katika hafla hiyo amewashukuru timu nzima iliyohusika katika kufanikisha mchakato huu hadi kufanikiwa wakiwepo wanasheria wa pande zote mbili na Property International.

Aidha aliahidi kutoa Afisa katika ofisi yake atakaekuwa akifuatilia utekelezaji wa mradi huu kila siku mpaka kukamilika kwake ambapo amesema mradi utakamilika ndani ya miaka 2 .

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe.Fatma Almas Nyangasa alimshukuru Rais Mhe.Samia Suluhu Hassan kwa maono yake ya kuifanya Tanzania yenye maendeleo kiuchumi na jitihada zake za kuifungua nchi kiuchumi na kuwaletea maendeleo watanzania na wanakigamboni tupo tayari kuunga mkono uwekezaji kwani tutanufaika na wingi wa ajira , kuongeza mapato na wawekezaji kusaidia jamii(CSR) kwa kurudisha faida kwa jamii.

Uwekezaji huu hadi kumalizika utagharimu Dola Bilioni 3,na Kwa awamu ya kwanza itatumika Dola milioni 400 kwa kujengwa Viwanda 50 Hadi kukamilika vitakuwa Viwanda 100.Eneo ni la square mita za mraba mil.2.2 litakuwa na huduma za jamii ndani,Viwanda vya nguo,madawa na vya kuunganisha magarizake.

# KIGAMBONI 2022

## Mbio za Mwenge wa Uhuru 2022 zilivyofana Kigamboni, Miradi yenye thamani ya Bilion.1.4 yapita bila kipingamizi.




*Viongozi wa Wilaya ya Kigamboni wakifurahiwa uwekwaji wa jiwe la Msingi na Mkimbiza Mwenge Kitaifa Sahil Geraruma kwenye ujenzi wa Bweni la wanafunzi lililojengwa kwenye Shule ya Sekondari kisarwe II*

Mwenge wa Uhuru 2022 Manispaa ya Kigamboni ulikimbizwa kilometa 103
katika Tarafa tatu (3) (Kigamboni, Somangila na Pembamnazi) na Kata saba (7) (Vijibweni,Kigamboni, Kibada, Kisarawe II, Pembamnazi, Somangila na Mjimwema) na ulipitia miradi ya maendeleo ya ujenzi minne (4) katika Sekta za Afya miradi miwili (2) (Uwekaji mawe ya msingi katika mradi wa ujenzi Kituo cha afya Tundwi Songani na Kichangani), Elimu mradi mmoja (1) (Uwekaji wa jiwe la msingi katika ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kike wenye mahitaji maalum shule ya Msingi chekeni Mwasonga), Barabara mradi mmoja (1) (Kuweka jiwe la msingi ujenzi wa Barabara ya Mikadi Beach – Shelaton).

Pia mwenge ulipitia kukagua shughuli za kikundi cha vijana cha TAMU Milk kinachojishughulisha na usindikaji wa maziwa pamoja na kikundi cha wanawake TUINUANE GROUP kinachojishughulisha na shughuli za uzoaji katika kata ya Vijibweni.

Miradi iliyopitiwa na Mwenge wa Uhuru mwaka 2022 ina thamani ya Tsh. 1.4 Bilioni zikiwemo Tsh. 54 milioni za michango na nguvu za wananchi, Tsh. 129 milioni za Mapato ya Ndani ya Halmashauri na Tsh.1.2 Bilioni fedha toka Serikali Kuu.

Aidha kwenye uwanja wa mkesha Mwenge wa Uhuru wa mwaka 2022 ulikagua mabanda mbalimbali ya shughuli za Kiuchumi na Kijamii ikiwemo mabanda ya mapambano dhidi ya dawa za Kulevya, mapambano dhidi ya Malaria,TAKUKURU, Vikundi vya Kiuchumi, Mfuko wa Afya ya Jamii, masuala ya Lishe, mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI na maandalizi ya sensa ya watu na makazi.

Mkimbiza Mwenge wa Uhuru kitaifa Mwaka 2022 Ndg. Sahil Geraruma aliridhia miradi yote na kuipongeza kigambaoni kwa kufanikisha utekelezaji wa miradi kwa kiwango kizuri.




*Viongozi wakiwa wameambatana na Mkimbiza Mwenge wa Uhuru Kitaifa Sahil Geraruma wakikagua ujenzi wa barabara ya mikadi beach kabla ya kuwekwa jiwe la msingi.*

# KIGAMBONI 2022

## Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhsimiwa Amos Makala aahidi kuboresha mazingira ya uwekezaji




*Mkuu wa Mkoa wa Dar -es-Salaam  Mheshimiwa Amosi Makalla akizungumza wakati alipotembela kiwanda cha ELSEWEDY kilichopo Kisarawe11  kuona namna kilivyojipanga kuwekeza Kigamboni.*

“Sisi kama Serikali ya Mkoa wa Dar es Salaam tunaahidi kuandaa mazingira mazuri ya uwekezaji ili wawekezaji wapate fursa ya kuwekeza.”

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mheshimiwa Amos Makala alipotembelea kiwanda cha kuzalisha vifaa vya umeme ikiwemo Transifoma Nyaya za umeme za ndani na nje ya nyumba cha Elsewedy kilichopo Kata ya Kisarawe II Manispaa ya Kigamboni.

Mheshimiwa Makala aliupongeza uongozo wa kiwanda hicho kwa kuwekeza katika Mkoa wa Dar es Salaam kwani uwepo wake utasaidia kupunguza gharama ya kuagiza vifaa toka nje ya nchi lakini pia na kuongeza ajira kwa vijana wa kitanzania.

Aidha katika ziara hiyo Mheshimiwa Makala alitoa wito kwa wawekezaji kuwekeza katika sekta ya nishati kwani fursa zipo nyingi hususani katika kipindi hiki ambapo Serikali inatekeleza sera ya kuhakikisha kila Kijiji kinapata nishati ya Umeme.

Katika ziara hiyo Mheshimiwa Makala pia alitembelea mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Mpira Pamoja na Mabweni yanayojengwa na shirikisho la soka Tanzania (T.F.F) ambapo ametoa wito kwa Shirikisho hilo kuanzisha shule za kukuza kipaji cha mpira wa miguu kwa vijana wadogo ili kuongeza chachu katika mchezo wa Soka.

**#UWEKEZAJI KIGAMBONI UNAWEZEKANA EWE MWANANCHI KARIBU KIGAMBONI KITOVU CHA UWEKEZAJI DAR ES SALAAM#**



*Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Amosi Makalla (kushoto) akizungumza na Diwani wa Kata ya kisarawe II ambapo kiwanda cha ELSEWEDY kimewekeza*

# KIGAMBONI 2022

## Mkuu wa Mkoa Amosi Makalla aridhishwa na utekelezaji wa miradi ya soko la kisasa kibada na Hospitali ya Rufaa ya kifua kikuu.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Amosi Makala awapongeza viongozi wa Wilaya ya Kigamboni kwa kusimamia vizuri utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya kifua kikuu sugu unaojengwa Vijibweni na Ujenzi wa Soko kubwa la Kisasa linalojengwa Kibada.

Pongezi hizo alizitoa Juni 15 alipokuwa kwenye ziara ya kukagua utekelezaji wa miaradi ya maendeleo na kusema kuwa Kigamboni imepata bahati ya kujengwa Hospitali ya Kifua Kikuu sugu kwa ukanda wa Mashariki na kwamba kwa muonekano wa ramani ya mradi wa ndani na n je unadhihirisha kuwa Hspitali itakua ya kisasa .

Mkuu wa Mkoa alisema kuwa tunapaswa kumshukuru Mhe. Rais kwa kutoa fedha kiasi cha Milioni 680 kwaajili ya utekelezaji wa mradi, alishukuru kuona unaendelea vyema na kuwataka viongozi wa Wilaya kuhakikisha wanamsimamia Mkandarasi ili aweze kukamilisha kwa wakati kama ilivyopangwa Oktoba 2022.

Kwaupande wa Soko la Kisasa la Kibada Mkuu wa Mkoa aliwapongeza viongozi kwa usimamizi mzuri na kuwataka kuhakikisha miundombinu ya kufikika inakua rahisi ili kuwasaidia wafanyabiashara watakaofanya kwenye soko hilo kuweza kukutana wa wateja wao moja kwa moja bila kizuizi chochote



Mkuu wa Mkoa wa Dar Es Salaam Mhe. Amosi Makalla akiwa ameambatana na Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe.Fatma Nyangassa (kulia) na wataalamu wa Manispaa kwenye ukaguzi wa ujenzi wa Hospitali ya kifua kikuu

"Wekeni miundombinu Rafiki,ikiwezekana wekeni kituo cha mabasi na barabara inayofikisha wananchi hapa moja kwa moja ili kuwasaidia wafanyabiashara wasipate hasara kutokana na kukosa wateja"Alisema Mkuu wa Mkoa.

Aidha Mkuu wa Mkoa pia aliwataka viongozi kuendelea kuwa wabunifu kwa kutazamia kujenga masoko mengine kwaajili ya wamachinga kwani Rais amekwisha onesha uthibitisho wa kuwapanga wafanyabiashara wakubwa na wadogo kwenye maeneo rasmi na mazuri ya kufanyia biashara.

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Fatma Nyangassa alisema kuwa ni soko la kwanza kubwa kiwilaya ambalo litasaidia wananchi kupata huduma ambazo kwa sasa wanalazimika kuzifuata kwenye Wilaya nyingine pia huduma zote zitapatikana sokoni hapo kwa kuwa na wafanyabaishara wakubwa na wadogo na Taasisi mbalimbali za kifedha.

Diwani wa Kata ya Kibada Mhe. Amini Sambo alimshukuru Rais kwa kuendelea kutoa fedha za utekelezaji wa mradi wa soko na kusema kuwa kuhusu miundombinu Mkurugenzi wa Manispaa alikwishaanza kushughulikia hususani wananchi walio na nyumba karibu na soko ili kuruhusu uwazi wa kufika kwenye soko kiurahisi.



***Muonekano wa Soko la Kisasa Linalojengwa Kibada.***

# KIGAMBONI 2022

## RC Makalla Aipongeza Kigamboni kwa kupata hati safi ,miaka 5 Mfululizo, aelekeza udhibiti wa mapato na 70% kuelekezwa kwenye Miradi ya maendeleo.

Mhe.Amosi Makalla aipongeza Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kwa kuendelea kupata hati safi kwa miaka mitano mfululizo na kuwataka kuendeleza mwenendo huo.

Mhe. Makalla alitoa pongezi hizi kwenye kikao cha Baraza maalumu la kupitia hoja za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwenye ukumbi wa Manispaa tarehe 28 Juni na kusema kuwa Halmashauri imejitahidi kuwa na hoja chache kwa mwaka 2021 kwani nyingi zilizopo ni za kipindi cha nyuma ambapo kati ya hoja 43, hoja 20 zimejibiwa na 23 zilizobaki kuhakikisha zinafanyiwa kazi kama ilivyoelekezwa.

Aliongeza kwa kusema kuwa pamoja na hati safi uongozi unapaswa kujikita katika kudhibiti upotevu wa mapato, kutumia asilimia 70 kwenye miradi ya maendeleo, kutumia asilimia 10 ya makundi maalumu na kutambua kuwa mwaka wa fedha ujao Serikali imeongeza asilimia 15 ya ukusanyaji mapato.

“Hatupaswi kutegema Serikali Kuu katika kutekeleza miradi wakati Halmasuari inao uwezo wa kukusanya mapato, tuhakikishe tunakusanya na kudhibiti upotevu wa mapato” Alisema Mkuu wa Mkoa.

Aidha Mkuu wa Mkoa aliagiza uongozi wa Manispaa kudhibiti biashara holela kwa wafanyabiashara kufanya kazi kwenye maeneo rasmi na kutunga sheria ndogo zinatazotumika kusimamia , kulipa fidia kwa wale wanaodai, kulinda maeneo kwa kuwekea mipaka, kudhibiti migogoro ya ardhi, kuondoa malalamiko ya wananchi juu ya dhuluma zinazofanywa na kampuni zinazouza ardhi kwa kuhakikisha wanafuata taratibu ili kuweze kuwahudumia Wananchi.



*Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Amosi Makalla wa kwanza kulia, Naibu meya wa Manispaa ya Kigamboni Mhe. Stephano Waryoba na Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni Erasto Kiwale wakifuatilia kwa makini uwasilishwaji wa Hoja za mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali*

Pia Mkuu wa Mkoa alizielekeza Taasisi zote zenye umiliki wa maeneo Kigamboni kuhakikisha wanasafisha maeneo yao na kuyawekea mipaka ili kuondoa mapori kwani Kigamboni ndilo eneo pekee Dar es Salaam lililobaki kwa kuendeleza ujenzi hivyo si vyema kuwa na mapori.

Kuhusu utekelezaji wa Anwani za makazi awamu ya Pili ya kuweka alama kwenye Nyumba na Barabara Mkuu wa Mkoa aliipongeza Kigamboni kwa kuendeleza vyema na kuwataka kumaliza zoezi vizuri huku wakiendelea kuhamasisha wananchi juu ya Sensa.

Mkuu wa Mkoa alitumia fursa hiyo pia kuwakumbusha wananchi juu ya zoezi la usafi linalofanyika kila mwisho wa mwezi na kusema kuwa kila mmoja aone anajukumu la kusafisha eneo lake kuanzia ngazi ya Kaya hadi kwenye maeneo ya kazi na biashara.

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Fatma Nyangassa amemshukuru Mkuu wa Mkoa kwa pongezi, kupokea maelekezo na kusema kuwa atahakikisha yote yanafanyiwa kazi ambavyo ameelekeza kwa kulenga kuongeza tija kwa maendeo ya Kigamboni ili kuweza kufikia malengo ya Serikali

# Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni awataka wananchi kuwa na utaratibu wa kupima Afya




***Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Fatma Nayangassa akizindua zoezi la afya cheki kwa kuanza kupima Afya yake kwenye moja la banda la watoa huduma lililokuwepo uwanjani hapo.***

Kauli hiyo aliitoa alipokuwa kwenye viwanja vya Mjimwema katika uzinduzi wa zoezi la upimaji wa afya bure ambapo Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe.Fatma Almas Nyangasa alikuwa Mgeni Rasmi.

Akiongea katika zoezi hilo litakalochukua siku mbili mfululizo Leo jumanne 7 Juni na jumatano 8 Juni Mhe.Nyangasa amewataka wananchi wa Kigamboni kujenga tabia ya kucheki afya zao mara Kwa mara ili kujitambua mapema iwapo wana maradhi katika miili yao ili kujitibia mapema kabla tatizo halijawa kubwa kwani ,Matatizo ya kiafya ni makubwa na changamoto hii imekua kutokana na kutofatilia afya zetu mara Kwa mara Kwa kuzichunguza ili kutatua tatizo mapema.

Mkuu wa Wilaya pia alitoa tahadhari katika kuendelea kujikinga na tatizo la Uvico 19 na kuwasihi kuendelee kuchukua tahadhari ikiwepo kupata chanjo ambayo ilipatikana pia katika zoezi hilo.

Aidha alimshukuru mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh.Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha kupatikana Kwa huduma hizi kupitia maagizo yake Kwa watendaji wake wa chini na uhusiano mzuri na wadau.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni Lucas David Ngamtwa,amewashukuru wadau waliojitokeza kutoa huduma bure,aidha amewasisitizia wananchi waendelee kufika kwani zoezi linaendelea ambapo kutakuwa na madaktari mbalimbali bingwa kutoka muhimbili watakaotoa huduma za uchunguzi wa afya.

Nae Naibu Meya wa Manispaa ya kigamboni Mhe.Stephano Warioba Kwa niaba ya Mstahiki Meya aliwashukuru watoa huduma ya kucheki afya,aliwataka wananchi kuzingatia ushauri watakaoupata ili kuepuka kupata matatizo zaidi pamoja na kufika kwa wingi kupima afya zao.

Wadau mbalimbali walishiriki kutoa huduma ya upimaji afya bure wakiwepo Management for Health Development ( MHD) ambao walitoa sapoti kubwa kuwezesha zoezi hilo lakini pia walitoa huduma ya utoaji chanjo ya Uvico 19, akiongea Mratibu wa chanjo kwa Wilaya ya Kigamboni Ndg.Martha Nkya wao alisema wako bega kwa bega katika kuunga mkono juhudi za serikali katika masuala ya afya ili kujenga taifa lenye watu wenye afya na kuleta maendeleo.



***Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Fatma Nyangassa akimsikiliza mmoja wa mwamanchi aliyefika kupata huduma kwenye afya cheki.***

# DC Fatma awataka wananchi kutambua ulinzi wa watoto ni la Jamii nzima.

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe.Fatma almasi Nyangassa aitaka jamii kutambua kuwa jukumu la ulinzi kwa watoto ni letu sote na hivyo ni vyema kuungana pamoja kutokomeza ukatili dhidi ya watoto.

Akizungumza kwenye hafla fupi ya maadhimisho ya siku ya mtoto wa Afrika kwenye viwanja vya shule ya msingi ya St.Joseph iliyopo kata ya Kibada Mhe.Fatma alisema kuwa mtoto anapaswa kulindwa bila kujali jinsia kwani malezi yameonesha watoto wa kike ndio waliopewa kipaumbele na wakiume kusahaulika .

Aidha aliwataka walimu,wazazi na walezi kuhakikisha wanatoa taarifa za kikatili zinazohusu watoto na kuacha tabia za kuwaficha wahalifu kwani kwa kufanya hivyo kunapelekea Serikali kushindwa kuchukua hatua na kumyima mtoto haki ya kisheria.

“Mtindo wa maisha umebadilika wazazi wamekuwa watafutaji na walimu wamekua na muda mwingi na watoto, naomba walimu tulindieni watoto hawa, nawewe mzazi hatakama mda mwingi unautumia kwenye kazi haizuii jukumu lako kama mzazi kuwa karibu na mtoto wako, jenga tabia ya kumsikiliza na kumsaidia anapohitaji msaada” Alisema

Mhe.Fatma.Aliongeza kwa kusema kuwa Serikali inamuangalia mtoto kwa jicho la mbali na ndiomaana kumekuwa na harakati za kumlinda hivyo jamii iungane katika jitihada hizo ili Taifa litengeneze watoto wanaojielewa na viongozi bora wa hapo baadae.

Mhe Fatma pia aliwataka watoto kuhakikisha wanakua wa kwanza kujilinda kwa kutoa taarifa



*Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe Fatma Nyangassa , Diwani wa Kata ya Mjimwema na watalaamu wengine wakipita kutazama ujumbe mbalimbali uliowasilishwa na watoto kupitia mambango.*



*watoto wa Shule ya Msingi Kibada wakipita na Bango kuonesha ujumbe wao katika kuadhimisha siku ya mtoto wa Afrika, katika viwanja vya Shule ya Msingi St.Joseph.*

kwa wazazi, walezi na waalimu pindi wanapoona dalili za kufanyiwa vitendo vya kikatili ikiwa ni pamoja na kuacha tabia ya kupokea vitu/zawadi kwa watu wasiowajua.

Kaimu mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni Bi.Happy Luteganya alisema kuwa kumekuwa na harakati nyingi za kumkomboa mtoto dhidi ya ukatili hivyo ameiomba jamii kuungana na Serikali chini ya Waziri Dorooth Gwajima ili kufikia azma ya kutokomeza kabisa.

Kwaupande wake Diwani wa Kata ya Mjimwema na mwenyekiti wa kamati ya huduma za jamii Mhe. omary Ngurangwa alisisitiza watoto kujitambua,kujilinda na kutoa taarifa dhidi ya vitendo vya kikatili kwani Taifa hili linawategema sana.

Maadhimisho haya yalijumuisha michezo mbalimbali , maigizo na upandaji miti.

# Wananchi watakiwa kuacha uchimbaji wa vifusi katika eneo la Mjimwema

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mheshimiwa Fatma Almasi Nyangassa amepiga marufuku shughuli zote za uchimbaji wa vifusi katika machimbo yaliyopo katika mtaa wa Mjimwema

Mheshimiwa Nyangassa ametoa kauli hiyo mchana wa leo alipotembelea eneo ilipotokea ajali ya watu kufukiwa na kifusi iliyotokea siku ya jumapili ambapo watu 3 walipoteza maisha.

Kwa upande mwingine Mkuu wa Wilaya ametoa muda wa siku tatu hadi kufukia jumamosi tarehe 09/04/2022 Wananchi wote wa eneo la machimbo kutoa mali zao zote na baada ya hapo ukaguzi utafanyika kuhakikisha eneo hilo linabaki salama.

Sambamba na hilo amewataka wananchi wote kuacha tabia ya kuuza kokoto barabarani na kuacha kuchimba vifusi hovyo hovyo ili kueupuka uharibifu wa mazingira ikiwa pamoja na kufuata maelekezo wanayopewa na Wataalamu.

Aidha Diwani wa Kata ya Mjimwema Mheshimiwa Omary Ngurangwa amesema kuwa eneo hilo si salama kwa shughuli ya uchimbaji na serikali ilishatoa maelekezo kuwa eneo hilo lisitumike.



*Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Fatma Nyangassa akizungumza na wananchi wanaojihusisha na uchimbaji wa vifusi Mjimwema, kushoto ni Diwani wa Kata ya Mjimwema Mhe.Omary Ngurangwa.*

Naye bwana Ally Maganga ambaye ni Afisa Madini wa Mkoa wa Dar es Salaam amesema kuwa hakuna biashara au liseni yoyote ya uchimbaji katika eneo hilo na amewataka Wananchi wanao taka kuchimba vifusi kuhakikisha wanapata liseni kutoka mamlaka husika



***Wananchi wanaojihusisha na uchimbaji vifusi walioshiriki kumsikiliza Mkuu wa Wialaya kwenye mkutano wa hadhara***

# DC Fatma Nyangassa awatoa hofu wazazi usalama wa chanjo ya polio kwa watoto

Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Fatma Nyangassa awataka wazazi kuwapeleka watoto wao kwenye vituo vya afya na kuwatoa kwenye nyumba zao pindi wahudumu wa afya wanapopita kutoa chanjo kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano kwani ni salama.

Mkuu wa Wilaya aliyasema hayo kwenye uzinduzi wa utoaji wa chanjo hiyo ulifanyika taraehe 18 Mei kwenye kituo cha afya cha kigamboni na kusema kuwa Tanzania haina bado ugonjwa huo lakini Serikali imechukua taahadhari baada ya jirani zetu kukumbwa na changamoto hiyo ili kuhakikisha watoto wanakua salama na afya njema.

Aliongeza kwa kusema kuwa wazazi watumie fursa hiyo kuwapatia watoto wao chanjo hiyo muhimu kwakufanya hivyo tutakuwa na uhakika wa usalama wa watoto kutoweza kupata tatizo hilo.

Aidha alisema kuwa chanjo hiyo haihusiani na chanjo nyingine zozote wataalamu wa afya wameelekeza chanjo nyingine zinaweza kuendelea wakati na ya polio ikitolewa bila kuleta madhara yoyote.

" Naomba mkawe mabalozi kwa wazazi wengine ili tuweze kufikia azma ya Serikali ya kuhakikisha watoto wote wanapatiwa chanjo hii, kwani,Serikali inaweka jitihada kubwa kuhakikisha watanzania wanakua salama katika mazingira yote." Alisema Mkuu wa Wilaya.

Mkuu wa Wilaya aliwashukuru wahudumu kwa kuendelea kutoa huduma nzuri mbali na changamoto na kuwataka kuendelea kuhudumia wananchi kwa kuangalia wagonjwa kwa jicho la ubinadamu ili waweze kutoa huduma za afya zenye tija inayozingatia utu na ubinadamu.



*Baadhi ya Wananchi walioshiriki kwenye uzinduzi wa zoezi la utoaji wa chanjo ya polio kwa watoto wenye umri kuanzia 0-5.*

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni DK.Lucas David Ngamtwa alisema kuwa Kigamboni imejipanga kuhakikisha watoto wote wanaostahili ya kupata chanjo wanapatiwa kwa watoa huduma kuhakikisha wanafikia kata zote 9 na Mitaa yake 67 ili kufikia azma ya Serikali ya kuwa na Taifa lenye Afya njema.

Irene Yakobo Mkazi wa Kigamboni alitumia fursa hiyo kuhamasisha wazazi kujitokeza ili kuwapatia watoto wao chanjo hiyo muhimu.



*Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Fatma Nyangassa (mwenye ushungi mwekundu) akishuhudia utoaji wa chanjo ya polio kwa watoto wenye 0-5 baada ya kufanya uzinduzi kwenye Hospitali ya Kigamboni.*

# KIGAMBONI 2022

## Kigamboni yapewa pongezi kwa utekelezaji wa Usafi.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Raisi Muungano na Mazingira Mhe. Selemani Jafo akimkabidhi cheti cha pongezi Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Fatma Almasi Nyangassa ishara ya kutambua juhudi zake katika kutekelezamasuala ya usafi.

Pongezi hizo zilitolewa katika zoezi la usafi wa jumamosi ya mwisho wa mwezi ambapo Wilaya ya Kigamboni kwa kushirikiana na Tanzania Environment and Empowerment (TEEMO) ambao wameunganisha tukio hilo na Maadhimisho ya mwezi wa Wanawake Duniani kwa kuungana na Wilaya ya Kigamboni katika usafi wa mwisho wa mwezi,ambapo mgeni rasmi alikuwa Waziri wa nchi ofisi ya Makamu wa Rais Muungano mazingira Mh.Selemani Jafo.

Katika tukio hilo Mh.Selemani Jafo alimkabidhi cheti cha pongezi Mh.Fatma Almas Nyangasa kwa kuwa mstari wa mbele katika harakati za usafi kwa Wilaya ya Kigamboni ,akikabidhi cheti hicho Waziri Jafo asema wanathamini juhudi za Mkuu wa Wilaya huyo katika kuhakikisha Kigamboni inakuwa safi,kwani amekuwa akitekeleza kwa asilimia mia moja agizo la Serikali.

Aliongeza pia katika masuala ya usafi ,alizitaka pia ofisi zingine za Serikali,Taasisi za serikali kutekeleza na kuhamasisha usafi katika maeneo yao ikiwepo maeneo ya masoko,stendi,maeneo ya mifereji na maeneo ya biashara na upandaji wa miti.

Aidha katika tukio hilo Mh.Waziri na Mkuu wa Wilaya wameshiriki kupanda miti ili kuendeleza utunzaji wa mazingira.Pia amezitaka Halmashauri zote kutekeleza agizo la kupanda miti mil.1.5 katika Halmashauri zao.

Nae Mkuu wa Wilaya akiongea katika hafla hiyo alishukuru kwa pongezi na aliahidi kuendeleza juhudi hizo katika kuunga mkono juhudi za Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh.Samia Suluhu Hassan za kutaka kupandwa miti na kuhamasisha usafi katika maeneo yetu.

Tukio Hilo limehudhuriwa na menejimenti ya Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kama ilivyo ada kushiriki katika usafi kila jumamosi ya mwisho wa mwezi.

### *# KIGAMBONI SAFI, WAJIBU WANGU#*



Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Fatma Almasi Nyangassa akishiriki zoezi la usafi  na viongozi wengine katika Hospitali ya Vijibweni.



Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kigamboni Mhe.Ernest Ndambo akishiriki zoezi la usafi na viongozi wengine kwenye Hospitali ya Vijibweni.

# KIGAMBONI 2022

## Wakulima Kigamboni wapewa mafunzo ya zao la Mbaazi na umuhimu wake kiafya.

Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa kilimo wameendesha mafunzo ya zao la kilimo cha zao la Mbaazi kwenye Bustani ya Gezaulole kwa lengo la kulitambulisha zao hilo na kuelimisha Wakulima na Wananchi umuhimu wa zao hilo na matumizi yake kwa ustawi wa afya ya binadamu lakini pia kujiongezea kipato.

Mkuu wa Idara ya Kilimo Ushirika na Umwagiliaji Bi. Priscilla Mhina amesema kuwa kupitia Idara yake walionelea ni vyema kulitambulisha zao la mbaazi kwa wakulima wa Kigamboni ili kuwanufaisha wakulima kwa kujiongezea kipato lakini pia kuimarisha afya ya mwili kutokana na faida ya kutumia zao hilo.

Katika mafunzo hayo wakulima waliwezeshwa kujua kanuni za kilimo ikiwemo za uchaguzi wa eneo kwa kilimo cha mbaazi, uandaaji wa shamba, uchaguzi wa mbegu bora, , upandaji wa mbegu husani kwa kutumia kitalu cha tray ili kuepukana

y



**Mkuu wa Idara ya Kilimo Bi.Priscilla Mhina (Kulia) akitoa mafunzo ya nadharia kwa wakulima wa Kigamboni walioshiriki mafunzo ya zao la mbaazi kwenye kito cha kilimo Gezaulole.**

na vimelea vitakavyoathiri mmea, matumizi sahihi ya mbolea na matumizi sahihi ya Dawa katika ukuaji wa zao la Mbaazi.

Akizungumzia faida ya zao la Mbaazi Afisa Lishe Mkoa wa Dar Es Salaam Bi. Anna Andrew amesema kuwa Mbaazi inasaidia kuongeza damu, kuwapa hamu ya kula watoto wanaosumbua kula, ni zao zuri kwa kushusha pressure na kusaidia watu wanaohitaji kupunguza uzito ikiwemo na kuimarisha misuli ya mwili.

Kwa upande wake Afisa kutoka shirika lisilo la Kiserikali la ADRA , Mama Dinabina amesema kuwa ushirikiano wa Serikali na Mashirika yasiyo ya Kiserikali ni mzuri kwani unasaidia kuwawezesha wananchi kupata fursa mbalimbali bila gharama yoyote ikiwemo ya zao la mbaazi ambalo limewawezesha kuwanufaisha watu wenye lemavu wa ngozi (Albino).

Teresia Januari ni Mkulima wa Kigamboni ,ameshukuru mafunzo yalitotolewa na kusema kwasasa kipaumbele kitakua ni zao la mbaazi kwani ameshatambua umuhimu wa zao hilo katika kuimarisha afya ya binadamu.

Mafunzo hayo yalikuwa ya siku moja ambapo yalihusisha mapishi ya aina mbalimbali yanayotokana na zao la Mbaazi.



Athumani MdoeAfisa kilimo msaidizi akiwaelekeza wakulima kuoteshea mbegu adhini

## Wajumbe wa Bodi za Usimamizi wa Vituo vya afya, Hosptali na Zahanati kufanya kazi kwa weledi



*Naibu Meya wa Manispaa ya Kigamboni Mhe. Stephano Waryoba ,Diwani wa kata ya Kisarawe II na Diwani wa Kata ya Kimbiji Mhe.Sanya Bunaya wakikabidhi kitabu cha mafunzo ya usimamizi wa vituo vya afya kwa mjumbe wa Bodi.*

Naibu Meya Manispaa ya Kigamboni Mheshimiwa Stephano Waryoba amewataka wajumbe wa bodi za usimamizi wa Vituo vya Afya katika Hospitali na Zahanati Manispaa ya Kigamboni kufanya kazi kwa weledi na kwa kujituma ili kutatua changamoto za kiafya kwa Wananchi.

Mheshimiwa Waryoba alitoa wito huo katika hafla fupi ya uzinduzi wa bodi za usimamizi wa Vituo vya Afya iliyofanyika Hospitali ya wilaya ambapo amewataka kufanya kazi kwa kuzingatia muongozo wa utekelezaji wa bodi hizo

Kwa upande mwingine Kaimu Mganga mkuu wa Manispaa ya Kigamboni Ndugu Iddy Kheri aliwataka wajumbe hao kuwa wazalendo kwa kubuni vyanzo vipya vya Mapato vitakavyosaidia katika upatikanaji wa vifaa tiba.

Kwa upande wake Mratibu wa Afya jamii wilaya ya kigamboni Bi. Dorice Batulaine aliwataka wajumbe wa bodi hizo kuonesha ushirikiano kwa wataalamu wa afya katika vituo wanavyosimamia na kuacha kufanya kazi kwa mazoea.

Bodi za usimamizi wa Vituo vya kutolea huduma za Afya zimeanzishwa kwa kuzingatia sheria kwa lengo la kuongeza chachu katika utoaji wa huduma za Afya

## Uhakiki wa Anwani za Makazi watakiwa kufanyika kwa Weredi

Kaimu Mkurugenzi Manispaa ya Kigamboni Ndg.Charles Lawisso Leo amefungua mafunzo ya Mfumo wa NAPA awamu ya pili kwaajili ya kuwajengea uwezo Watendaji wa Kata,Mitaa na Wakusanya data kuweza kutekeleza vyema Uhakiki wa Anwani za Makazi.

Akifungua mafunzo hayo 30 Juni kwenye ukumbi wa Manispaa amewasisitiza washiriki hao kuwa makini ili zoezi la Uhakiki wa Anwani liweze kutekelezeka kwa ufanisi.

Aidha alitumia fursa hiyo kuwakumbusha wananchi wa Kigamboni kufika kwenye ofisi za za Mitaa ili kuweza kuhakiki taarifa zao na kufanya marekebisho ikiwa yatakuwepo.

Aliendelea kwa kusema kuwa Anwani za makazi ni zoezi linaloendelea likilenga kurahisisha zoezi la Sensa ya watu na Makazi linalotarajiwa kufanyika August 23 , pia Anwani hizi zitarahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Mafunzo hayo yaliwezeshwa na Maafisa kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Wizara ya Habari na mawasiliano.



*Mratibu wa Anwani za Makazi na Postikodi Kigamboni Magdalena Malunda akizungumza na washiriki wa mafunzo ya Uhakiki wa Anwani za makazi.*

# KIGAMBONI 2022

## Vijana 100 waliofuzu mafunzo ya kilimo cha kisasa katika kituo cha kilimo cha Gezaulole Kigamboni watakiwa kutumia ujuzi huo kujiajiri



Vijana wakiwa kwenye kwenye mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa mfumo wa nadharia na vitendo

Tarehe 30/3/2022 wanafunzi 100 waliokuwa wakipatiwa mafunzo ya mbinu Bora za kilimo cha kisasa walifuzu mafunzo hayo katika kituo cha Rasilimali kilimo kilichopo Manispaa ya Kigamboni Gezaulole.

Akiongea mara baada ya kufunga mafunzo hayo ya awamu ya pili Ndg Prisilla Mhina alisema Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Kitengo cha vijana na ajira waliandaa programu ya kuwawezesha vijana katika kila Halmashauri ambapo vijana wamekuwa wakinufaika kupata mafunzo ya kilimo cha kisasa na namna ya kujenga kitalu nyumba,kuihudumia na kuitumia na kisha kujiongezea kipato kwa kujiajiri kupitia kilimo.

Mkuu wa Idara ya Kilimo aliwataka kuyatumia kwa vitendo mafunzo waliyoyapata



Vijana wakiwa kwenye mafunzo ya nadharia ya kilimo cha mboga mboga kwa kutumia kitalu

ili lengo la mafunzo litimie ,kwa kwenda kujiunga katika vikundi na kutumia fursa zilizopo za mikopo na kuanzisha kilimo biashara kwa pamoja ili kujiajiri na kujiongezea kipato. Mafunzo hayo yalitolewa kwa njia ya nadharia na vitendo ambapo waliweza kufundishwa kuhusu utengenezaji wa Kitalu nyumba,visumbufu vya mazao na namna ya kuvizuia ili kukuza uzalishaji na kuongeza tija katika kilimo.

Hii ni awamu ya pili mafunzo hayo kutolewa ambapo Vijana hao waliwezeshwa mafunzo hayo bila gharama yoyote .

***#KIJANA SHIRIKI KIKAMILIFU SENSA YA WATU NA MAKAZI AGOSTI 23 KWA MAENDELEO YAKO#***

# KIGAMBONI 2022

## SENSA KWA MAENDELEO JIANDAE KUHESABIWA

### SENSA NI NINI??

Sensa ya Watu na Makazi ni utaratibu wa kukusanya, kuchakata, kuchambua na kusambaza taarifa za kidemografia, kiuchumi, mazingira na kijamii za watu wote na makazi yao katika nchi kwa kipindi maalum.

Utaratibu huu huwezesha kupata takwimu za msingi kama idadi ya watu wotekwenye nchi kwa umri na kwa jinsi; hali zao za elimu; ajira; mahali wanapoishina taarifa nyingine ambazo huwezesha Serikali Kufuatilia na Kutathmini Mipango ya maendeleo ya Taifa.

### SENSA ITAFANYIKAJE??

Tarehe 23-28 Agosti 2022, Karani wa Sensa atafika katika kaya akiwa na Dodoso la Sensa na kuuliza maswali ambayo yatajibiwa na Mkuu wa Kaya au mtu mwingine yeyote katika kaya ambaye ana taarifa za kaya na wanakaya waliolala ndani ya kaya husika usiku wa kuamkia siku ya Sensa.

Ikumbukwe watakaohesabiwa ni watu wote bila kujali uraia wao ilimradi walilala ndani ya mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania usiku wa kuamkia siku ya Sensa

Sensa haihusishi watu kutoka katika kaya zao kwenda kwenye kituo maalum kwa ajili ya kuhesabiwa, badala yake watu watabaki katika kaya zao na kuendelea na shughuli zao, au baadhi ya watu tu wanaweza kubaki katika kaya ilimradi wahakikishe wanazo taarifa zote za wanakaya na watu wote.

### FAIDA YA SENSA YA WATU NA MAKAZI

Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 kama zilivyo sensanyingine zilizotangulia itatoa majawabu katika mambo yamsingi yanayohusu watu **kiafya, kielimu, kijamii, kimazingira na kiuchumi.**

Upimaji wa mipango mbalimbali ya Serikali hutegemea taarifa zinazotoka na aidha na Sensa au Tafiti ambazo chimbuko lake ni Sensa ya Watu na Makazi.

Katika nchi nyingi, Sensa ya Watu na Makazi ni chanzo pekee cha Takwimu za Kidemografiaambazo hutumika kupanga na kufuatilia utekelezaji wa mipango ya maendeleo endelevu ya Wananchi katika Sekta zote za kiuchumi, Kijamii na Mazingira kama vile sekta ya elimu,Afya, Mazingira na pia zina mchango mkubwa katika kupunguza umaskini.

### 1.ELIMU SENSA HUSAIDIA

# Maamuzi ya wapi shule ijengwekutokana na wingi wa watoto wenyeumri wa kwenda shule
# Idadi ya walimu unaozingatia uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi
# Idadi ya madarasa, matundu yavyoo na miundombinu ya huduma za usafi shuleni kulingana na wingi wa wanafunzi
# Mahitaji ya vifaa vya kufundishia kama vile vitabu, tablets na vitendea kazi vingine

### 2.AFYA SENSA HUSAIDIA

#Maamuzi ya wapi kituo cha afya kijengwe kutokana na wingi wa watu
#Idadi ya wahudumu wa afya unaozingatia uwiano wa watu
#Idadi ya wakunga au wahudumu wa afya waliopata Elimu ya ukunga na uzazi wa mpango
#Mahitaji ya vifaa tiba na dawa

# KIGAMBONI 2022
## HABARI KATIKA PICHA



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Amosi Makalla akiwa pamoja na Viongozi wa Wilaya na TEMESA kwenye ziara yake ya kukagua mwenendo wa Vivuko vya Kigamboni.



Wajumbe wa ziara ya Kamati ya Fedha wakiwa kwenye picha ya pamoja mara baada ya kutembelea miradi mbalimbali ya maendeleo.



Muonekano wa Vizimba vya Soko la Kisasa la Kibada linalotarajiwa kuhudumia wafanyabiashara kuanzia wadogo hadi wakubwa ambapo hadi kukamilika kwake Bilioni 6.1 zitakuwa zimetumika.



Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe.Fatma Nyangassa akiwa ameambatana na wataalamu wa manispaa kukagua miundombinu ya Soko la Feri.

**Limeandaliwa na;**
**Alda Phestor Sadango**
**Afisa Habari.**



**HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**
**S.L.P 36009, DAR ES SALAAM**
**www.kigambonimc.go.tz**